

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU “LABOUR CLINICS” KWA AJILI YA
KUSIKILIZA NA KUTATUA KERO ZA WAFANYAKAZI NA WAAJIRI**

1. Kama mnavyokumbuka, mnamo tarehe 29 Januari, 2021 nilizindua mkoani Morogoro Mpango Kazi ujulikanao kama “*labour clinic*” kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za wadau wa Sekta ya Kazi wakiwemo waajiri na wafanyakazi. Kwa kuzingatia Mpango huu Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Kazi imeweka utaratibu wa kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi kuwa ni siku ya kukutana na kuzungumza na wadau kwa lengo la kutatua kero na malalamiko yao.
2. Mpango huu umeanza kutekelezwa tangu tarehe 29 Januari, 2019 ambapo siku hiyo katika Ofisi za Kazi za mikoa nchi nzima Wataalam na Watendaji mbalimbali waliendesha vikao kati yao na waajiri, wafanyakazi na wadau ili kutoa fursa ya kupokea kero na malalamiko yao.
3. Kutokana na umuhimu wa Mpango huu katika kumaliza malalamiko ya wadau, nimeona nitumie fursa hii kuwakumbusha wadau wa sekta ya kazi kuwa utaratibu unaendelea na keshokutwa tarehe 26 Februari, 2021 kwenye Ofisi za Kazi za Mikoa nchi nzima wataalam na watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu watakutana na wadau kuwasikiliza na kutatua changamoto zao. Hivyo, nitoe rai kwa waajiri, wafanyakazi na wadau wa masuala ya kazi kwa ujumla kufika katika Ofisi za Kazi za Mikoa ili kuwasilisha kero, changamoto na ushauri.
4. Ninawaagiza Maafisa Kazi. Watendaji na wataalam wote wanaohusika katika zoezi hilo kuhakikisha mnatoa muda wa kutosha kwa wadau kueleza kero na changamoto zinazowakabili.

5. Nitoe rai kwa wadau kutumia fursa hii muhimu ambayo Serikali imeweka ili muweze kuwa mnapata majibu ya kero zenu bila kulazimika kusafiri huku na huko kutafuta huduma hiyo.

Imetolewa na;



Jenista J. Mhagama (Mb)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU
(SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU)**

24/02/2021